

Maswali

1. Nani walikuwa wakipigana na Waisraeli?
2. Nani aliuawa kwa Mlima wa Gilboa?
3. Waisraeli walifanya nini walipojua kwamba Sauli amekufa?
4. Samweli alipaka nani mafuta awe mfalme wa pili?
5. Daudi alienda kuishi wapi?
6. Daudi alitaka kujengea Mungu nini huko Yerusalemu?
7. Mungu alisema nani atamjengea Hekalu?
8. Mungu aliahidi wana wa Daudi nini?
9. Mungu aliahidi nini juu ya mzao mmoja wa Daudi?
10. Yule mzao ni nani? Hii ahadi itatimizwa lini?

Majibu

1. Wafilisti walikuwa wakipigana na Waisraeli.
2. Sauli, Yonathani na wana wengine 2 wa Sauli waliuawa.
3. Waisraeli walitoroka?
4. Samweli alipaka Daudi mafuta awe mfalme wa pili.
5. Daudi alienda kuishi Yerusalemu.
6. Daudi alitaka kujengea Mungu Nyumba kule Yerusalemu.
7. Mungu alisema mwana wa Daudi, Sulemani atamjengea Hekalu.
8. Mwana mmoja (mzao) wa Daudi, atatawala kama mfalme Yerusalemu.
9. Mmoja wa mzao wa Daudi atatawala kutoka Yerusalemu milele.
10. Yesu atatawala milele kwa Ufalme wa Mungu duniani atakaporudi hapa duniani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



28 Daudi ni mfalme

Marejeo

1 Samweli 31: 1 – 6; 2 Samweli 7:16

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alipenda Daudi na akaahidi kwamba mmoja wa wana wa Daudi atatawala juu ya Ufalme wake milele.

Maneno maalum

- 28.1 Wafilisti + Mlima wa Gilboa + Sauli na wana 3 + uawa + Waisraeli + toroka
- 28.2 Samweli + paka mafuta + Daudi + mfalme
- 28.3 Daudi + Yerusalemu + Mungu abariki + jenga jumba la mfalme + nyumba ya Mungu + Sulemani atajenga Hekalu
- 28.4 Mungu aliahidi + Daudi na wanawe + wafalme wa Yerusalemu + mzao mmoja + tawala milele + Yesu + rudi + tawala mataifa yote + milele



28. 1 Waisraeli na Wafilisti walikuwa wakipigana tena. Walikuwa wanapigania kwa Mlima wa Gilboa. Wafilisti walikuwa wanashinda vita. Wafilisti waliona Sauli na watoto wake watatu, kwa hivyo walianza kuwafuata mbio. Waliua Yonathani na ndugu zake wawili. Sauli alipigwa na mshale na kuumizwa sana. Sauli alijua atakufa lakini hakutaka auawe na Wafilisti. Aliuliza mchukua silaha zake amuue kwa upanga. Mchukua silaha hakukubali kumuua, kwa hivyo Sauli alijirusha kwa upanga wake na akafa.

Waisraeli walipojua kwamba Sauli na wanawe watatu wamekufa, waliogopa sana. Walifikiri kwamba Wafilisti watakuja na kuwaua. Walitoka kwa nyumba zao na kwa miji na kutoroka. Wafilisti walienda na kuishi kwa nyumba za Waisraeli. Daudi aliposikia kwamba Sauli na wanawe wamekufa, alihuzunika sana. Alilia sana kwa ajili ya rafiki yake Yonathani.

28.2 Daudi alikuwa ametawazwa na Samweli kama mfalme hapo awali kabla ya haya. Waisraeli walipojua kwamba Sauli alikuwa amekufa, waliendea Daudi kule Hebroni. Walimwambia kwamba wao walikuwa watu wake naye alikuwa mfalme wao. Daudi alitawazwa tena kama mfalme kule Hebroni.

28.3 Daudi alienda kuishi Yerusalemu baada ya kutawazwa kama mfalme. Aliifanya Yerusalemu kuwa mji mkuu wa Israeli. Wakati mwingine Yerusalemu huitwa “Mji wa Daudi.” Daudi aliendelea kuwa maarufu kwa sababu Mungu alikuwa naye na alimbariki.



Yerusalemu

Daudi alijijengea jumba la mfalme na za watu wake kule Yerusalemu. Siku moja alikuwa amekaa kwa jumba la mfalme na akafikiria na kutaka kujengea Mungu nyumba. Lakini Mungu alimwambia kwamba si yeye atajenga ila ni mtoto wake Sulemani ndiye atajenga hiyo nyumba – Hekalu.

28.4 Mungu alimwambia atambariki. Mungu alimwambia kwamba wana wake na wana wao watakuwa wafalme Yerusalemu. Mungu alimwahidi kwamba mzao wake mmoja atatawala kwa kiti cha Daudi cha enzi kule Yerusalemu, na Ufalme wake utakuwa wa milele.

Mungu hutimiza ahadi zake, kwa hivyo tunaongoja huo Ufalme. Ni Ufalme wa Mungu wenye Yesu atakuja kusimamisha hapa duniani atakaporudi. Yesu atakapokuja atatawala akiwa kwa kiti cha Daudi kule Yerusalemu. Atatawala juu ya falme zote za ulimwengu na Ufalme wake utakuweko milele. Huwa tunaomba hayo tukisema Sala ya Bwana: “Ufalme wako uje, mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani.....”